

# **MAJIBU YENYE FAIDA**

**NO. 13**

**(KUHUSU MASWALI YA MIFUMO MIPYA)**

**MTUNZI: SHEIKH SWALEH BIN FAWZAN ALFAWZAN**

**MFASIRI: ABUL AALIYAH UMAR BIN MUHAMMAD KONDO**

**\*PONGWE -TANGA-TANZANIA\***

\*\*\*\*\*

\*\*\*\*\*

## **Swali la kumi na sita.**

Makaundi ya Da'wah yamekuwa mengi hivi sasa,na walinganizi kwenye Dini ya Allah (pia) wamekuwa wengi,lakini (kwa masikitiko makubwa) muitikio ni mdogo,basi kuna siri gani katika hilo?

**Jawabu :** Tunasema (hivi):

**Mosi.** Sisi hatuhamasishi juu ya wingi wa makundi katika Da'wah na mengineyo,sisi tunataka jama'a moja ya kweli inayolingania kwenye Dini ya Allah kwa Elimu.

Ama wingi wa makundi,na wingi wa mifumo,basi haya ni mionganini mwa yanayosababisha kufeli na mvutano,na Allah –hali ya kuwa ametukuka-anasema: *{Wala msizozane mkaingiwa woga, na zikapotea nguvu zenu<sup>1</sup>}*.

---

<sup>1</sup> -Surat-ul -Anfaal ( 46)

Na amesema ‘Azza wa Jalla: {*Wala msiwe kama wale walio farikiana na kukhitalifiana..<sup>2</sup>*}

Na amsema-hali ya kuwa umetukua utajo wake-

{*Na shikamaneni kwa Kamba ya Allah nyote pamoja, wala msifarikiane<sup>3</sup>.*}

Tunataka jama’ah moja itakayokuwa juu ya mfumo (njia) sahihi na Da’wah sahihi,hata kama watafarikiana(watakuwa mbalimbali) katika miji hakika marejeo yao ni moja na baadhi watawarejea wengine,na baadhi watatoa kwa wengine hili ndilo linalotakiwa.

Ama wingi wa makundi ambayo hayakuwa juu ya mfumo (manhaj) moja basi marejeo yake ni kukhitalifiana.

---

<sup>2</sup> -Surat-ul-Aali ‘Imraan (105)

<sup>3</sup> -Surat-ul-Aali ‘Imraan (103)

**Pili:** Hakuna shaka ya kwamba, mlinganizi kuwa na ikhlaasi kunamuathiri mwenye kulinganiwa.

Basi atakapokuwa mlinganizi ni mwenye kuitakasa nia yake na akawa analingania juu ya mfumo sahihi kwa Utambuzi na Elimu katika kile anachokilingania, kwa hakika huyu atamuathiri mwenye kulinganiwa.

Ama akiwa hana ikhlaasi katika kulingania kwake, na hakika si vingine analingania kwenye maslahi yake binafsi, au analingania kwenye uchama (uhizbi) au kwenye kundi lililopinda au kwenye ta'ssubi hata kama alikuwa anajiita muislamu hakika huyu hanufaishi kitu chochote na hakuna chochote anachokilingania kwenye uislamu.

Na hivyo hivyo atakapokuwa anawalingania watu kwenye Kitabu cha Allah na Sunna za Mtume – swala na salamu zimshukie- lakini hayafanyii kazi

yale anayoyalingania,basi hili pia ni katika mambo yanayowakimbiza watu kuwa mbali na yeye,na Allah ndiye ambaye anajua yaliyomo ndani ya nyoyo, na anayajua anayoyafanya mtu yejote katika sehemu yoyote, basi atakapokuwa anapambana na Allah kwa kumukhalifu anapokuwa faragha, na anapodhihiri mbele za watu anawalingania kwenye kheri na hali ya kuwa yeye yuko kinyume na kheri hiyo,basi hili halitaathiri chochote wala halitakubaliwa kwa sababu Allah hakujalia katika ulinganizi wake (huyu) baraka.

Hebu waangalie walinganizi wenye ikhlaasi imetoa matunda gani da'wah yao na hali ya kuwa wao ni mmoja mmoja na wana wapinzani (wengi..!)

Mfano: (wa hao walinganizi wenye ikhlaasi) Shaikh-ulislami ibn Taymiyyah,na wanafunzi wake,na

sheikh Muhammad bin ‘Abd-il-Wahhabi na wengineo.

Na angalia wingi wa walinganizi leo, na wingi wa makundi ya ki-Da’wah, na uchache wa athari zao na uchache wa kunufaisha kwao ili ujue kuwa mazingatio ni kwa namna ya ulinganizi si kiasi cha ulinganizi.